**HALMASHAURI YA WILAYA CHALINZE**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MANDERA**

**S.L.P 85, CHALINZE**

**Barua pepe: *mandera1girls@gmail.com***

**Tovuti: *www.mandera.sc.tz.***

**Simu: *0768498022/0784775583***

**Ndugu:_______________________________________________**

**<u>YAH: MAAGIZO YA MWANAFUNZI ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO MANDERA SEKONDARI MWAKA 2025</u>**

Kwa niaba ya wafanyakazi wa shule ya sekondari ya wasichana Mandera, nafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2025 **HONGERA SANA**. Shule hii ipo katika Kata ya Mandera, Tarafa ya Miono, Halmashauri ya Chalinze,kilometa mbili (02) kutoka barabara kuu ya Chalinze – Tanga

(Barabara kuu iendayo Moshi na Arusha) unateremkia kijiji cha kwanza baada ya kuvuka Mto Wami ukiwa unatokea Chalinze ila kama unatokea Tanga ni kabla ya kuvuka mto Wami, kijiji hicho kinaitwa Mandera Kibaoni. Baada ya hapo unafuata barabara iendayo **SAADAN NATIONAL PARK**. Ukipanda basi liendalo Miono,unateremkia shuleni kabisa, shule ipo upande wa kushoto wa kanisa la **ROMAN CATHOLIC** Parokia ya Mandera.

**MAHITAJI YA LAZIMA YA MWANAFUNZI YA KURIPOTI NAYO**

**A. SARE YA SHULE**.

i. Sketi 02 ndefu rangi ya kijivu mpauko mshono wa Rinda Box (**urefu acha inch 5 kutoka kwenye unyayo) ifike kwenye kifundo cha mguu**
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi (Wanafunzi Waisilamu washone Nusu kanzu).
iii. Tai ndefu mbili rangi ya kitambaa cha sketi ya shule (kijivu mpauko) kwa mwanafunzi asiyevaa nusu kanzu.
iv. Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye soli fupi vya kupiga rangi na kufunga na Kamba .(Bajaji, simpo na raba haziruhusiwi).
v. Aje na soksi nyeupe ndefu jozi nne.

**vi.** Sweta la kijivu rangi ya sketi ya shule (kijivu mpauko)

**vii.** Nguo ya kushindia kitambaa aina ya ESTEEMY NAMBA 1 rangi ya Maroon (damu ya Mzee) ashone gauni refu mshono wa rinda Box **(urefu acha inch 5 kutoka kwenye unyayo).**

viii. T-shirt yenye nembo ya shule inapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi elfu kumi na tano tu (15,000/= )

ix. Aje na truck – suit rangi ya kijivu kama rangi ya sketi ya shule kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa masomo ya usiku (PREP)

x. Aje na jezi rangi nyekundu (bukta nyekundu ndefu hadi magotini na taiti nyeusi ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu) kwa ajili ya Michezo.

xi. Aje na raba nyeupe au nyeusi kwa ajili ya michezo

xii. Aje na sanduku (Tranka) linalofungwa kwa kufuli kwa ajili ya kuhifadhi vitu vyake kwa usalama.

xiii. Aje na begi jeusi kwa ajili ya kubebea daftari darasani

**B. VIFAA VINGINE.**

i. Aje na jembe kwa ajili ya usafi.

ii. Aje na kikombe, kijiko na sahani ya bati yenye sehemu ya kuwekea chakula na mboga (sahani na kikombe viwe vya **Bati** na **SIO** Plastiki wala mfupa).

iii. Aje na ndoo mbili ndogo za plastiki (AZIANDIKE JINA LAKE).

iv. Aje na shuka mbili za rangi ya Pinki (hata kwenye duka la shule yanapatikana).

v. Aje na net (chandarua) rangi nyeupe ya pembe nne futi 3 pamoja na godoro la futi 3

vi. Aje na faili 1 ya plastic (spring file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake za mitihani.

vii. Nguo za nyumbani haziruhusiwi ila aje na kanga 2, taulo 1, nguo za ndani yaani taiti 3, chupi zisipungue 6, singlet 2, blazia 3 ( rangi ni nyeupe/nyeusi isipokuwa chupi rangi yoyote) na nguo za kulalia rangi ya pink(Night dress).

viii. Aje na tochi, inasaidia punde umeme unapokatika ghafla

ix. Kwa mwanafunzi skauti aje na vazi rasmi la skauti

x. Aje na shuka zito (blanketi jeusi) kwa mwenye matatizo ya kifua. **SIO LAZIMA**

xi. Aje na madaftari ya kutosha yasiyopungue 15 (counter books), Rula, kalamu za risasi, kalamu za wino (pen) na mathematical set (mkebe).

xii. Mwanafunzi aje na Kadi ya Bima ya afya.

xiii. Simu ya Mkononi pamoja na vifaa vinavotumia Umeme haviruhusiwi shuleni.

**C. MAAGIZO MUHIMU**

- Mchango wa chakula ni Tsh 410,000/= kwa mwaka, ukiweza kulipa yote kwa mkupuo ni vizuri zaidi. Vinginevyo unaweza kulipa Tsh 205,000/= kama malipo ya nusu mwaka ambapo utatakiwa kulipa kiasi hicho mara mbili kwa mwaka au Tsh 102,500/= kama malipo ya robo mwaka na hivyo utatakiwa kulipa mara nne kwa mwaka kiasi hicho cha fedha ili kufikia lengo la kiwango cha fedha unachotakiwa kulipa kwa mwaka.
- Fedha zote hizi ziingizwe kwenye akaunti ya shule yenye namba **21101100023 NMB** Jina la Akaunti ni **MANDERA GIRLS REVENUE COLLECTION**. Fedha

  Taslimu (Cash) hazipokelewi shuleni.
- Mwanafunzi anatakiwa afike shuleni tarehe **……………………..** siku ya Jumatatu kuanzia saa 02:**00 Asubuhi** na muda wa mwisho kuripoti shuleni ni **saa 10:30 jioni**. zaidi ya hapo mwanafunzi hatapokelewa mpaka siku itakayofuata.
- Tarehe ya mwisho ya mwanafunzi kuripoti itakuwa **……………………** na siku za kuripoti ni siku za kazi tu.
- Mwanafunzi atawajibika kufuata taratibu na sheria zote za shule pindi awapo shuleni mara tu baada ya kupokelewa.
- Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule kama ilivyoelekezwa kwenye kipengele cha sare za shule wakati wa kuripoti.

Pamoja na fomu hii yenye maelekezo, zimeambatanishwa fomu nyingine tatu ambazo zinatakiwa kusomwa kwa umakini na kufanyiwa kazi:-.

i. **Fomu ya hospitali,** (iliyoandikwa kwa kiingereza) Ijazwe kwenye hospitali ya serikali na kugongwa muhuri.

ii. **Fomu ya mkataba**, isomwe kwa umakini na kujazwa panapotakiwa.


iii. **Fomu ya maelezo binafsi**, ijazwe pia kwa umakini

iv. **Sheria za shule.** Isomwe na mwanafunzi kwa umakini kabla hajaripoti shule

Fomu zote hizi zirudishwe shuleni mwanafunzi anaporipoti

Kwa mara nyingine tena tuna kukaribisha na kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako na tunakusihi uitumie nafasi hii vizuri kwa faida yako, familia yako pamoja na Taifa lako kwa ujumla.

**UKIMWELIMISHA MTOTO WA KIKE UMEELIMISHA JAMII**



**-------------------------**

**REGINA A NGEREZA**

**MKUU WA SHULE**




## MKATABA WA MWANAFUNZI KUKAKAA HOSTELI

Shule ya Sekondari ya Wasichana Mandera ni shule ya kutwa ila imebahatika kuwa na Hosteli/Mabweni.

Mwanao atalazimika kukaa Hosteli kwa kuwa katika shule hii hakuna mwanafunzi wa kutwa/anaelala nyumbani hivyo Mzazi/Mlezi utawajibika kumhudumia mwanao awapo hapa shuleni na hasa kwa gharama ya chakula ambayo ni Tsh: 410,000/= kwa Mwaka mzima au Tsh:

205,000/= kwa muhula {miezi 6) au 102,500/= Kwa robo Muhula.

Mzazi/Mlezi utajaza mkataba wa shule wa kuwa tayari kumhudumia mtoto wako muda wote atakaokua anasoma katika shule hii. Endapo utashindwa au hauko tayari basi unaruhusiwa kumuhamisha mtoto wako kwenda shule nyingine yoyote ya kutwa.

Michango hiyo ya chakula iingizwe katika Akaunti Namba **21101100023 NMB Jina la Akaunti**

**MANDERA GIRLS SECONDARY SCHOOL REV.**

# MKATABA.

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………………………….. kidato cha …………………………………… 2024. Nimesoma Mkataba huu na kuuelewa na nimeridhia kuchangia huduma hizo za chakula na pia naahidi kuwa nitachangia kwa wakati bila kuleta

usumbufu wowote kwa uongozi wa kamati ya Wazazi ili mtoto wangu aweze kupata huduma ya Chakula kadri inavyostahili. Na endapo nitashindwa kutekeleza ahadi yangu hii basi mimi mwenyewe natamka kwamba nitalazimika Kumhamishia mwanangu shule nyingine ya kutwa.

Jina la Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………………

Sahihi yake ……………………………………………………………………………..

Namba ya Simu; …………………………………………………………………….

Jina la Mwenyekiti wa wazazi (Anapatikana shuleni) **ELIBARIKI SAZIA**

Sahihi yake: …………………………………………………………………………….

Namba ya Simu: **0686880847**

## TAARIFA BINAFSI

Jina la Mwanafunzi: ………………………………………………………………………

Jina la Mzazi: ……………………………………………………………………………..

Kijiji: ……………………………………………………………………………………
kata:……………………………………………………………………………………….

Tarafa:………………............................................................................................................

Anuani kamili : ………………………………………………………………………………

Simu ya mzazi: ……………………………………………………………………

Wilaya..………………………………………………………………………………

Mkoa: ………………………………………………………………………….....

1. **Majina ya Watu watano wanaoruhusiwa kumtembelea/kumchukua Mtoto awapo shuleni.**

| S/N | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | ANUANI |
|---|---|---|---|
| **1** | | | • **S.L.P …………………………** <br> • **SIMU …………………………** |
| **2** | | | **S.L.P…………………………..** <br> **SIMU …………………………..** |
| **3** | | | • **S.L.P …………………………..** <br> • **SIMU ……………………………** |
| **4** | | | • **S.L.P ………………………..** <br> • **SIMU ………………………..** |
| **5** | | | • **S.L.P ………………………..** <br> • **SIMU ……………………........** |

2. Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Jina: ………………………………………………………… Sahihi: …………………………

3. Kijiji cha ………………………………………………………………………………**...**

Jina na Sahihi ya Afisa Mtendaji wa kijiji

Jina: ………………………………………………………… Sahihi: ………………………

Namba ya simu ya Mtendaji wa Kijiji ……………………………………………………………

## SHERIA MUHIMU ZA SHULE

- Sheria na kanuni za shule zinazingatia misingi ya heshima , adabu, uaminifu, utii na tabia njema kwa ujumla.
- Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kwa ajili ya mafanikio katika masomo na malezi mema.
- Mwanafunzi atasimama anapomsalimia Mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri,hii ikiwa ni wageni mbalimbali pamoja na watumishi wote wa Shule.

1. Ni marufuku kwa mwanafunzi;
   a) Kunyoa kipara.
   b) Kusuka nywele
   c) Kumpiga mwenzake au kupigana
   d) Kutia nywele dawa na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa.
   e) Kuvaa kofia, viatu vyenye soli nene (vya ghorofa) au mapambo mengine akiwa shuleni.
   f) Kumiliki simu ya mkononi, line/kadi ya simu pamoja na vyombo vya kutumia umeme mfano redio pasi katika eneo la Shule.
   g) Kusinzia au kulala darasani
   h) Marufuku kwa mwanafunzi kutembea anapohitajika mahali ( anatakiwa kukimbia)
   i) Kutunza nguo, viatu, ndoo, mifagio na vitu vingine visivyohusika darasani
2. Mwanafunzi atasimama kwenye msitari wakati wa kupata huduma yoyote.
3. Lazima mwanafunzi ahudhurie na awahi mahali anapotakiwa katika shughuli za Shule.
   a) Na ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa.
   b) Ahudhurie prepo, vipindi vya dini na vipindi vya darasani kwenye chumba alichopangiwa.
   c) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu zoezi la kupandishwa na kushushwa kwa bendera ya Taifa
   d) Kila mwanafunzi ahudhurie na kushiriki katika michezo mbalimbali.
4. Ni lazima mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na kitambulisho kwa nyakati zifuatazo:
   a) Anapohudhuria masomo darasani na wakati wote awapo shuleni.

b) Anapotoka nje ya Shule kwa ruhusa maalum kwenda benk, posta, hospitali au kwa shughuli yoyote itakayomlazimu kwenda nje ya shule.

c) Mwanafunzi anaruhusiwa kuvaa track suit (avae tishati kwa ndani) wakati wa prep usiku na si wakati mwingine.

d) Mwanafunzi atavaa jezi wakati wa michezo tu (bukta urefu hadi magotini na taiti nyeusi ndefu kwa ndani)

e) Mwanafunzi atavaa nguo ya kushindia baada ya muda wa masomo na wakati wa prep ya usiku

f) Mwanfunzi anaruhusiwa kuvaa jezi wakati wa michezo na si wakati mwingine.

5. Ni lazima mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya Shule wakati wote, isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya Shule kwa ruhusa maalum pia mwanafunzi haruhusiwi kuonana au kuongea na mzazi au ndugu yeyote katika eneo la Shule pasipo ruhusa ya Mwalimu.

6. Hairuhusiwi kuleta au kupokea vyakula kutoka nje ya Shule, hii ni kwa ajili ya usalama wa wanafunzi asije akala chakula kisichofaa.

    - Hairuhusiwi kuingia na wala kuhifadhi chakula chochote bwenini

7. Taarifa zote muhimu kutoka kwa Wazazi /Walezi mfano kifo au matatizo ya kifamilia zipitie kwa Mkuu wa Shule /Makamu Mkuu wa Shule.

8. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini na dawa, kibiriti, mshumaa, kamba kisu au kitu chenye hatari kinachoweza kuhatarisha maisha.

9. Huduma za kiafya zinapatikana katika zahanati iliyo karibu na Shule. Iwapo kuna mwanafunzi aliyeandikiwa dawa na daktari mara afikapo shuleni dawa zote zipelekwe kwa matron(mama mlezi wa wanafunzi). HAKUNA HUDUMA KWA WAGONJWA WA MASHETANI NI VYEMA MWENYE TATIZO HILI AKASOMA SHULE ZA KUTWA.

10. Wazazi/Walezi pamoja na ndugu watawatembelea watoto wao mara moja (1) kwa mwezi (kwa miezi isiyokua na likizo) yaani Jumapili ya mwisho wa mwezi na kama siyo siku ya kuwatembelea hutoruhusiwa kuonana na mtoto wako , muda ni kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa 10.00 jioni.

    Ukichelewa hutoruhusiwa kumwona. Tafadhali zingatia muda.

11. kwa Wazazi/Walezi mara ufikapo shuleni kwa ajili ya tatizo lolote huruhusiwi kuongea na mwanao au kumpa vitu au fedha pasipo idhini ya mwalimu, tafadhali nenda ofisini uweze kusaidiwa shida yako na si vinginevyo.

12. Mwanafunzi awapo shuleni mawasiliano na mzazi yafanyike kupitia simu ya mkuu wa shule na simu za shule amabazo ni:- **0655760446, 0676760446, 0749991446 na 0762740446 zenye usajili wa jina la NICODEMUS AUGUSTINO.**

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

1) wizi
2) Uasherati, ubakaji , ushoga na usagaji
3) Ulevi, kuvuta sigara au bangi na kutumia madawa ya kulevya. 4) Kupiga ama kupigana na mtu mwingine.
5) Makosa yote ya jinai(criminal offences) kama vile kujaribu kujiua, kutishia wengine kwa silaha mfano kisu au sumu.
6) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma mfano kuandika madawati, kuta, milango au vitabu vya shule.
7) Kudharau bendera ya Taifa, kukufuru sehemu ya ibada kwa dini au dhehebu lolote 8) Kuolewa.
9) Kupata au kutoa mimba
10) Kuchocheana/ kuvuruga Amani na usalama.
11) Kugoma/Kukataa adhabu.
12) Kutokuwepo shuleni kwa muda mrefu bila taarifa au maelezo yanayokubalika.
13) Kutoroka, kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa au kulala nje ya shule.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA.

PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO: The Medical Officer (Government Hospital)

…………………………………………….

From: Mandera Girls Sec .School
P.O Box 85
Chalinze
Date …………………………

Mr/Mrs/Miss …………………………………………… (Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time Secondary Education. The examination should include the following ineligible in case of a defect. Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate ineligible for a secondary education.

1. (A)Eye sight (B)Speech (C)Hearing (D)Limbs(E)Venereal Disease(F)Leprosy(G)Epilepsy 2. Neuroses (3) pregnance 4.Other serious diseases

**Part** B MEDICAL CERTIFICATE

1. a) Eye sight ……………………………………………………………..

b) Hearing ……………………………………………………………..

c) Speech ……………………………………………………………

d) Limbs ……………………………………………………………

e) Venereal disease …………………………………………………………

f) Leprosy …………………………………………………………

g) Epilepsy ……………………………………………………………

2. Neuroses ……………………………………………………………

3 Pregnancy ………………………………………………..................

4. Other serious disease ……………………………………………………………

I have examined the above named and consider that she is in physically fit and mentally fit for full time secondary education

Designation …………………………………………date……………………

Signature & Official stamp (To completed by a government Officer)

**NB**.

In case of any serious health problem (s) the record from the government hospital must be submitted to school while reporting.